

Mpango wa Familia Zilizofanikiwa

Mei 2008

Mpango wa Familia Zilizofanikiwa una huduma za familia zenye mapato ya chini. Hizi ni pamoja na zifuatazo:

- Msaada wa kifedha, unaojulikana pia kama Msaada wa Muda wa Familia (TAF)
- Huwasaidia watu wazima na shida zao za kupata kazi
- Hutoa huduma ya msaada wa kazi, mafunzo, shughuli za kazi, na elimu

Mpango huu husaidia familia kujifunza ustadi mpya, kuongeza uwezo wao wa sasa, na kuweka watoto manyumbani mwao.

Kupokea msaada kutoka kwa Mpango wa Familia Zilizofaulu, familia lazima iwe na angalau mtoto mmoja nyumbani aliye na umri wa chini ya miaka 18. Mtoto huyu huenda akawa hajazaliwa. Mtoto huenda akawa anaishi na mzazi au jamaa. Mtoto huyo huenda pia anaishi na mtu aliyetajwa na korti amlee mtoto huyo, kama vile mlezi, mhifadhi, au mtunzaji.

Familia lazima ziwe na mapato ya chini na rasilimali chache. Mapato ya washirika wote wa familia nyumbani huhesabiwa. Aina zingine za mapato na rasilimali hazihesabiwi, kama:

- Nyumba ambayo familia inaishi
- Mali chini ya \$2,000
- Magari
- Fanicha, vitu vya kibinafsi, na vifaa vingine
- \$90 pamoja na asilimia 60 ya mapato

Familia huenda zikapata msaada wa kifedha wanapokuwa wakitafuta kazi maadamu wanafikia mahitaji ya mpango. Hii ni pamoja na kushirikiana na Mpango wa Msaada wa Watoto. Familia zinaweza kupata TAF kwa miezi 60 tu katika maisha yao. Familia zinazopata TAF huenda pia zikapata manufaa ya matibabu na ulezi wa mtoto.

Viwango vya manufaa ya kifedha vinategemea mapato ya familia. Inategemea pia jimbo ambalo familia inaishi. Chati iliyo hapo chini inaonyesha manufaa ya juu kabisa ya kifedha ambayo ukubwa wa familia unaweza kupokea.

Malipo ya Msaada wa Kifedha				
Ukubwa wa Familia	Mkoa wa Mashambani	Mkoa wa Mashambani wenye Gharama ya Juu	Mikoa Yenye Watu wengi	Mikoa Yenye Watu Wengi yenye Gharama ya Juu
1	\$224	\$229	\$241	\$267
2	\$309	\$314	\$326	\$352

3	\$386	\$391	\$403	\$429
4	\$454	\$459	\$471	\$497
5 au zaidi	Ongeza \$61 kwa kila mtu wa ziada			

Familia zinaweza kupata aina zingine za huduma za misaada ili kusaidia katika kuziandaa kufanya kazi. Huenda zikapata huduma hizi za msaada zinapokuwa bado zikipokea msaada wa kifedha. Huduma hizi zinaweza kuendelea kwa mwaka baada ya kuacha kupokea msaada wa kifedha. Familia huenda zikapokea huduma na misaada kadhaa, pamoja na zifuatazo:

Usaidizi wa kupata na kutunza kazi
 Ujuzi wa kazi
 Huduma za ulemavu wa kusoma, shida za dawa au pombe, au mzozo wa kinyumbani
 Huduma za kusaidia kusoma na kuhesabu
 Huduma za afya ya kiakili
 Matibabu ya kimwili
 Usaidizi wa kuvumiliana na ulemavu
 Usaidizi wa uzazi
 Usaidizi wa kupata meno bandia, miwani, vifaa vya kusaidia kusikia
 Mafunzo ya kazi
 Usaidizi wa kupata GED au kujifunza Kiingereza
 Usaidizi wa kufika maeneo ya kazi
 Mavazi
 Msaada wa mahitaji muhimu
 Gharama ya kuhama kunaohusiana na kazi

Watu wazima lazima wafanye mojawapo ya yafuatayo ndiposa kupokea msaada wa kifedha wa familia yao:

Wawe kazini au katika shughuli za kikazi
 Wawe katika mipango ya kusaidia kupunguza viziwi vya kufanya kazi
 Wawe wanamlea mtoto chini ya umri wa miaka 6
 Wawe wanamlea mmoja wa kaya ambaye ni mlemavu
 Watu ambao hawahitajiki kupata kazi au kuwa katika shughuli za kikazi huenda wakaomba huduma.

Maombi

[Bonyeza hapa](#) ili kufikia maombi ya huduma zetu. Kwa huduma zingine, au kupata Ofisi ya Jamii na Urekebishaji tabia au Eneo la Kufikia lililo karibu na wewe, tumia viungo vilivyo mwisho wa ukurasa huu.

Rudi kwa Ukurasa wa maskani ya EES

Ukurasa Ulisasishwa: Oktoba 20, 2008